

**MULIKA Na. 43 (2)**

**DESEMBA 2024**

**JARIDA LA TAASISI YA TAALUMA ZA  
KISWAHILI**

**MHARIRI MKUU  
Mussa M. Hans**

**MHARIRI MSAIDIZI  
Leonard F. Ilomo**

**ISSN 0856-0129  
e-ISSN 2546-2202**



©TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI 2023

**Mhariri Mkuu**

Dkt. Mussa M. Hans, Idara ya Lughya ya Kiswahili na Isimu, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

[mussahans30@gmail.com](mailto:mussahans30@gmail.com)

**Mhariri Msaidizi**

Dkt. Leonard F. Ilomo, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

[leonardilomo@gmail.com](mailto:leonardilomo@gmail.com)

**Bodi ya Uhariri**

Dkt. Mussa M. Hans, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

[mussahans30@gmail.com](mailto:mussahans30@gmail.com)

Dkt. Leonard F. Ilomo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

[leonardilomo@gmail.com](mailto:leonardilomo@gmail.com)

Dkt. Ramadhani T. Kadallah, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

[Kadallahr@yahoo.com](mailto:Kadallahr@yahoo.com)

Prof. Shani O. Mcchepange, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

[shaniom@yahoo.co.uk](mailto:shaniom@yahoo.co.uk)

Dkt. Lutz Diegner, Chuo Kikuu cha Humboldt, Ujerumani

[lutz.diegner@asa.hu-berlin.de](mailto:lutz.diegner@asa.hu-berlin.de)

Dkt. Athuman Ponera, Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania

[atponeraman@gmail.com](mailto:atponeraman@gmail.com)

Dkt. Miriam Kenyani Osore, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya

[kenyanimo@yahoo.com](mailto:kenyanimo@yahoo.com)

**Washauri wa Wahariri**

Prof. Abdulaziz Lodhi, Chuo Kikuu cha Uppsala, Sweden

[Abdulaziz.lodhi@lingfil.uu.se](mailto:Abdulaziz.lodhi@lingfil.uu.se)

Prof. Sangai Mohochi, Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya

[smohochi@gmail.com](mailto:smohochi@gmail.com)

Prof. Cyprean Niyomugabo, Chuo Kikuu cha Rwanda

[niyomugabocyprien@gmail.com](mailto:niyomugabocyprien@gmail.com)

Prof. Method Samwel Semiono, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Tanzania

[methodsamwel16@gmail.com](mailto:methodsamwel16@gmail.com)

Prof. Ipara Odeo, Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya

[ideo@kibu.ac.ke](mailto:ideo@kibu.ac.ke)

Prof. Alwiya Saleh Omar, Chuo Kikuu cha Indiana, Bloomington-Marekani

[alwiyahuseina@gmail.com](mailto:alwiyahuseina@gmail.com)

Prof. Beata Wojtowicz, Chuo Kikuu cha Warsaw, Poland

[b.wojtowicz@uw.edu.pl](mailto:b.wojtowicz@uw.edu.pl)

Dkt. Wael Nabil Ibrahim, Chuo Kikuu cha Al Azhar, Misri

[wael\\_nibrahim@hotmail.com](mailto:wael_nibrahim@hotmail.com)

Dkt. Felix Kwame Sosoo, Chuo Kikuu cha Ghana, Ghana

[munguanipenda@yahoo.com](mailto:munguanipenda@yahoo.com)

**ADA KWA MWAKA<sup>1</sup>**

Kwa Taasisi	US \$ 40 pamoja na usafiri
Kwa Mtu Binafsi	US \$ 20 pamoja na usafiri
Jina la Akaunti	University of Dar es Salaam
Namba ya Akaunti	012105005554
Jina la Benki	National Bank of Commerce
Tawi la Benki	UDSM Branch
Msimbo wa Benki	255
Msimbo wa Utambulisho	NLCBTZTX
Bei ya Jarida kwa Tanzania	ShT 10,000

**Habari za Mkondoni**

Makala katika jarida hili yanapatikana pia katika tovuti za [www.udsm.ac.tz](http://www.udsm.ac.tz); [www.ajol.info](http://www.ajol.info) na <https://mft.ebscohost.com>. Aidha, ikitirisho za jarida hili zinapatikana katika tovuti ya Chama cha Ukuzaaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU) kupitia tovuti ya [www.chaukidu.org/mulika](http://www.chaukidu.org/mulika).

**Kwa mawasiliano tumia anwani ifuatayo:**

**Mhariri Mkuu, MULIKA**

**Taasisi ya Taaluma za Kiswahili-Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**S.L.P. 35110,**

**Dar es Salaam.**

Baruapepe: [mulika1970@udsm.ac.tz](mailto:mulika1970@udsm.ac.tz); [mulika.udsm@gmail.com](mailto:mulika.udsm@gmail.com)

**Hakimiliki**

Hakimiliki © Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa wala kutoa makala ya jarida hili kwa njia yoyote ile bila idhini ya mchapishaji, isipokuwa kwa nukuu fupi kwa ajili ya utafiti au matumizi binafsi, mapitio ya kitaaluma au mjadala kwa kuwarejelea waandishi wa makala husika.

---

<sup>1</sup> Ada hizi ni kwa nakala ngumu kwani nakala tepe zinapatikana bila malipo.

## Taarifa kwa Waandishi wa Makala

### **Usuli na Mawanda**

*MULIKA* ni jarida la taaluma ya Lugha na Fasihi ya Kiswahili. Jukumu lake kuu ni kukusanya na kusambaza maarifa yanayohusu Lugha na Fasihi ya Kiswahili yaliyokitwa katika utafiti mpevu. Kutowana na mahitaji kwa baadhi ya watumiaji wa Kiswahili katika nyanja nyingine, hivi sasa jarida hili linapokea pia makala yaliyoandikwa kwa Kiswahili lakini yenyenye maudhui mengine nje ya Lugha na Fasihi ya Kiswahili. *MULIKA* limeendelea kuwa daraja kati ya watumiaji wa Kiswahili popote walipo, na wataalamu wa Kiswahili katika shule za sekondari na vyuo vya elimu ya juu Afrika ya Mashariki na kwingineko.

### **Uandaaji na Utumaji wa Makala**

Jarida linapokea makala yaliyoandikwa kwa Kiswahili TU. Makala yapigwe chapa katika muundo wa *Microsoft Word*, mistari ikitengwa kwa kipimo cha nafasi ya 1.5 baina ya mstari na mstari na pambizo liwe na upana toshelevu. Ukurasa wa kwanza wa makala uoneshe jina la makala, jina kamili la mwandishi (au waandishi) wa makala (ikiwa ni pamoja na wadhifa wake), anwani na baruapepe yake. Ukurasa wa pili uoneshe jina la makala na ikisiri isiyozidi maneno 250. Makala yawe na ukubwa wa maneno kati ya 4000-8000 na mapitio ya vitabu maneno 800-1200.

### **Upitiaji na Uhariri wa Makala**

Makala yoyote kabla ya kuwasilishwa yawe yamepitiwa vema na mwandishi na kufanyiwa uhariri wa kina kuhakikisha kwamba hayana makosa ya kiuandishi na kimaudhui. Mwandishi anapaswa pia kuhakikisha kwamba taarifa zote zilizomo ndani ya makala ni sahihi na vyanzo vya taarifa hizo ni vyenye kuaminika.

### **Urejeleaji**

Unapotaja marejeleo kwenye matini, taja jina la mwisho la mwandishi, likifuatiwa katika mabano na tarehe ya chapisho lake na kurasa zilizorejelewa, k.m. Yahya (1983:139). Kwenye orodha ya marejeleo au bibliografia majina ya warejelewa yapangwe kialfabeti. Tanchini na tanmwisho ziwekwe namba na zitumike pale tu inapobidi. Maelezo ya tanmwisho yatolewe kwenye ukurasa wa pekee mwisho wa makala, yaani kabla ya kuorodhesha marejeleo.

Majina ya vitabu, majorida na anwani za tasnifu/tazmili viandikwe kwa italiki. Majina ya makala yawekwe ndani ya alama za kufunga na kufungua semi kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

### **Kitabu**

Massamba, D.P.B. (2017) *Historia ya Kiswahili: Mtazamo Mpya 100 KK hadi 2000 BK*. Dar es Salaam: Kiswahili Development Limited.

### **Sura ya Kitabu**

Hamisi, A.M. (2008) "Filosofia za Sera za Lugha". Katika J.G. Kiango (Mh.) *Maendeleo ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI. kur. 78-100.

### **Makala ya Jarida**

Majariwa D. (2021) “Upenyezaji na Ukubalifu wa Mkururo wa Konsonanti katika Fonolojia ya Kiswahili: Mifano katika Maneno Yaliyopokelewa kutoka Kiingereza na Kiarabu”. *Mulika*, Juz. Na. 40 (1): 1-23.

### **Makala ya Jarida la Mkondoni**

Omari, S. (2019) “Gender Representation in Simba and Yanga’s Joking Cartoons in Tanzania”. *Eastern African Literary and Cultural Studies*. Juz. 5(2): 79-93. Inapatikana katika <https://doi.org/10.1080/23277408.2019.1643606>. Ilisomwa tarehe 12 Juni 2012.

### **Tasnifu/Tazmili Isiyochapishwa**

Peterson, R. (2014) *Matumizi na Dhima za Lugha katika Mandhari-lugha ya Jiji la Dar es Salaam*. Tasnifu ya Uzamivu (Hajachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Saalam.

### **Gazeti**

Duwe, E. (2018) “Zijue Sifa za Kufundisha Kiswahili Nje ya Nchi”. *Mwananchi*. 16 Oktoba 2018. uk. 13.

### **Mifano na Vielelezo ndani ya Makala**

Mifano yote, majedwali, michoro, ramani na picha mbalimbali vipangwe kwa uwazi na unadhifu kwenye kila ukurasa kadiri vliviyotumika. Taarifa zote hizo zinapaswa kutumika kwa kuzingatia kanuni za maadili ya kazi ya kitaaluma. Mathalani, ni muhimu kuweka chanzo thabiti cha taarifa inayoingizwa kwenye makala, iwe ni picha, michoro, mifano na vingine vinavyohusiana na hivyo. Kwa ujumla, data zinazotumiwa katika makala ni lazima ziwe thabiti na zenye kuaminika.

### **Udanganyifu wa Kitaaluma**

Kunakili maneno, mawazo, michoro, n.k., kutoka vyanzo vingine bila kubainisha vyanzo husika kutafasiriwa kuwa ni udanganyifu wa kitaaluma na hiyo inaweza kuwa mionganoni mwa sababu za makala yako kukataliwa. Ikiwa itabainika kuwa makala yaliyochapishwa katika jarida yamekiuka maadili ya kazi za kitaaluma, taratibu za kisheria zitachukuliwa kulingana na kanuni na miongozo iliyopo.

### **Ridhaa ya Kuchapisha**

Ikiwa makala yatakubaliwa, mwandishi wa makala ataandikiwa barua kupewa taarifa hiyo. Mwandishi wa makala atapaswa kuthibitisha kwa maandishi kwamba makala hayo hayajachapishwa wala kutumwa mahali pengine. Taarifa hiyo itachukuliwa kuwa ni idhini ya makala hayo kuchapishwa katika Jarida la *MULIKA*.

### **Mchakato wa Kutathmini Makala**

Makala ya *MULIKA* yatatathminiwa na wasomaji wasiopungua wawili ambao watafanya kazi hiyo bila kufahamu taarifa za mwandishi. Waandishi wanatakiwa kuepuka kuonesha utambulisho wowote unaowahuusu ndani ya makala ili kuwawezesha wanaoyatathmini kufanya kazi yao kwa haki. Sifa mojawapo ya watu watakaotathmini makala ni weledi katika uwanja unaofanyiwa tathmini.

Mbali na kutumwa kwa watu wa kutathmini, makala yatapitiwa pia na wahariri wa jarida ili kuhakikisha kwamba yametimiza mahitaji ya jarida kabla ya kuendelea na hatua inayofuata.

Miongoni mwa vipengele vitakavyozingatiwa wakati wa kutathmini makala ni walengwa wa makala, lengo la makala, mapitio ya maandiko, nadharia, mpangilio na uwasilishaji, ufanuzi wa maudhui, uasili na uzingatiaji wa maadili, matumizi ya michoro na picha, uandishi wa matini na marejeleo.

Endapo maudhui ya makala yatakidhi mawanda na sera za jarida, makala yatatumwa kwa watathmini wawili ambao hawajulikani kwa mwandishi, kuwaomba kukubali kuyatathmini makala. Watathmini watatathmini miswada wakilenga kuangalia ubora wake katika maudhui, uwazi wa uwasilishaji, uasili, mchango wake kitaaluma na uzito wake kimaudhui na kiutafiti. Watathmini watapatiwa mwongozo utakaowaongoza wakati wa kutathmini makala. Baada ya kupata maoni ya watathmni, wahariri watapitia maoni hayo kabla ya kuyatuma kwa waandishi wa makala ili kuhakikisha kwamba maoni yaliyotolewa yanaendana na mwongozo uliotolewa. Baada ya maoni hayo kupitiwa na wahariri kujiridhisha kwamba yanaendana na mwongozo wa jarida, yatatumwa kwa waandishi wa makala ili waweze kuyafanya kazi kisha kurejesha mswada uliozingatia maoni yaliyotolewa na watathmini wa makala. Wakati wa kurejesha makala baada ya kufanya kazi maoni, mwandishi wa makala atapaswa kuandaa jedwali linaloonesha maoni aliyopewa na namna alivyoyafanya kazi.

Kutokuzingatia mwongozo wakati wa kuandaa makala kunaweza kuwa sababu ya makala kutopewa nafasi katika hatua za awali za tathmini. Aidha, kutokuzingatia makataa ya kufanya marekebisho kwa waandishi wa makala kunaweza kuwa sababu ya makala hayo kutokuzingatiwa katika toleo husika.

Waandishi ambao makala yao yatakubaliwa mbali na kuandikiwa barua kujuzwa hatua ya kukubaliwa kwa makala hayo, watatumwa nakala tepe ya makala yao pamoja na kurasa za awali zinazoonesa taarifa mbalimbali za jarida kwa marejeleo.

Jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba maoni yaliyomo kwenye makala yaliyochapishwa katika jarida hili ni ya waandishi wa makala na si lazima yakubaliane na yale ya Wahariri au Bodi ya Uhariri ya Jarida la *Mulika* na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili kwa ujumla wake.

**YALIYOMO**  
**UKURASA**

Taarifa kwa Waandishi wa Makala.....	iv
Mchakato wa Kutathmini Makala.....	vi
Yaliyomo.....	vii
Tahariri.....	viii
Waandishi wa Makala.....	xi
Uchanganuzi wa Kirai Kihusishi cha Kiswahili <i>Tumaini Mahendeka na Luinasia E. Kombe.....</i>	197
Mikakati ya Urekebu wa Kiswahili kama Lugha rasmi Nchini Kenya <i>Mogden Chisia, Iribe Mwangi, Ayubu Mukhwana, na Hezron Mogambi...</i>	211
Makosa ya Kimofolojia ya Watumiaji wa Kiswahili na Sababu zake: Uchunguzi Kifani wa Watumiaji wa Kiswahili na Kihaya <i>Anold Kamugisha.....</i>	235
Uhusiano wa Wapemba na Wamakonde: Hoja za Kihistoria <i>Pendo Mwashota na Mussa Hans.....</i>	257
Miundo ya Vishiriki vya Kitenzi Isiyofuata Udarajia wa Dhima za Kisemantiki katika Sentensi za Kiswahili <i>Oliva Mang'ita na Fabiola Hassan.....</i>	277
Uakisikaji wa Udongo kama Suala la Kiikolojia katika Ushairi wa Kiswahili: Mfano kutoka Ushairi wa Mohammed na Mberia <i>Mugwe Mwaniki, Omboga Zaja, na Rayya Timammy.....</i>	307
Mla: Kiunzi cha Uzingatizi wa Maadili ya Waswahili katika Methali Teule za Kiswahili <i>Martina Duwe.....</i>	321
Uchunguzi wa Mtagusano baina ya Hisia na Motifu: Mfano kutoka Tamthiliya ya Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe <i>Winfid Mligo, Aldin Mutembei, na Ramadhani Thomas Kadallah.....</i>	336
Urithi wa Vivuli: Kufichua Nyuzi za Baada ya Ukoloni katika Riwaya ya <i>Nguu za Jadi</i> <i>Waithiru Kago Antony.....</i>	351

## TAHARIRI

Kwa mara nyingine, jarida la MULIKA Na. 43(2) linakueletea mfululizo wa makala kutoka kwa waandishi mbalimbali. Toleo hili lina jumla ya makala 9 yanayohusu maeneo mbalimbali ya taaluma za Kiswahili. Waandishi wa makala haya wanatoka ndani na nje ya nchi ya Tanzania.

Makala yaliyoandikwa na Tumaini Mahendeka na Luinasia E. Kombe yanahu su uchanganuzi wa kirai kihusishi cha Kiswahili. Katika makala haya, waandishi wamebainisha muundo wa kirai kihusishi cha Kiswahili, wameeleza sifa za kumuundo za kirai kihusishi na kufafanua sababu za kiisimu zinazowafanya wataalamu wa Kiswahili watofautiane kuhusu muundo na uchanganuzi wa kirai kihusishi ilhali wanatumia mkabala mmoja wa sarufi miundo virai. Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Sarufi Miundo Virai ambayo inachambua na kuonesha viambajengo vya virai. Makala haya yanaonesha kwamba kirai kihusishi kinaundwa na kihusishi kama neno kuu na kirai nomino au kishazi tegemezi kama vijalizo vyake. Pia, makala yanaonesha kuwa sifa za kumuundo za kirai kihusishi ni neno kuu la kirai kutawala vijalizo vyake na neno kuu kutosimama peke yake. Aidha, yanabainisha kwamba sababu za kiisimu zinazowafanya wataalamu wa sarufi ya Kiswahili watofautiane kuhusu uchanganuzi wa vijenzi vya kirai kihusishi ni athari za tafsiri kutoka katika lugha ya Kiingereza na kutozingatiwa kwa kanuni za miundo virai.

Mogden Chisia, Iribi Mwangi, Ayubu Mukhwana, na Hezron Mogambi wameandika makala inayohusu mikakati ya urekebu wa Kiswahili kama lugha rasmi nchini Kenya. Katika makala yao waandishi hawa wamebainisha mikakati ambayo Kiswahili kinatumia kukua ili kufanikisha dhima yake mpya nchini Kenya kwenye mawasiliano rasmi. Data ya zilizotumika katika makala haya zimetokana na maandishi mbalimbali kuhusu matumizi na urekebu wa lugha pamoja leksikoni kutoka *Kamusi Pevu ya Kiswahili* (2016). Makala yaeongozwa na Nadharia ya Saikolojia ya Kijamii. Katika makala haya imebainishwa kuwa Kiswahili kinatumia mikakati mbalimbali ya urekebu wa kifonolojia pamoja na ule wa kisemantiki ili kupata msamiati na istilahi za kusahilisha na kufanikisha mawasiliano. Ili kuhakikisha usahihi wa leksikoni zinazokopwa na kutoholewa, makala haya yametoa mapendekezo ya kuundwa kwa chombo mahususi cha kitaifa ambacho kitasimamia shughuli zote zinazohusiana na ukuzaji wa msamiati na maendeleo ya Kiswahili kwa ujumla pamoja na kutumiwa kwa Kiswahili katika mawanda yote, yakiwamo yale rasmi, ili kiweze kurekebu na kuyafanikisha majukumu yake mapya ya kimawasiliano kama lugha rasmi nchini Kenya.

Naye Anold Kamugisha ameshughulikia makosa ya kimofolojiaya watumiaji wa Kiswahili na sababu zake, akijikita kuchunguza watumiaji wa Kiswahili na Kihaya. Katika makala hayo, mwandishi amebainisha makosa kadhaa yanayojitokeza ambayo ni pamoja na kuongeza viambishi visivyohitajika, uchanganyaji msimbo, matumizi ya ngeli zisizo sahihi, uhawilishaji wa maneno kutoka Kiingereza, na matumizi ya maumbo ya lughatandawazi. Aidha, makala yamebainisha sababu za mbalimbali za kutokea kwa makosa hayo. Miongoni mwayo ni kutojua vyema Kiswahili, athari ya Kihaya, tafsiri isiyo sahihi, na ufanano wa kimuundo wa maneno ya Kiswahili na Kihaya. Aidha, inabainishwa kuwa makosa haya huathiri uwezo wa kumudu ruwaza sahihi za lugha. Hivyo, mwandishi, katika makala haya, anasisitiza umuhimu wa kujifunza ngeli za nomino ili kuepuka kubananga Kiswahili na kuzingatia sarufi sahihi na utamaduni wa jamii.

Katika makala yanayohusu uhusiano wa Wapemba na Wamakonde, waandishi, Pendo Mwashota na Mussa Hans, katika kueleza uhusiano huo, wameegemea hoja za kihistoria. Makala haya yametumia data zilizokusanywa kwa njia ya usaili, hojaji, na ushuhudiaji katika maeneo ya Kisiwa cha Pemba na katika mkoa wa Mtwara. Wakichambua data kwa kuongozwa na Nadharia ya Mwachano na Makutano ya lugha za Kibantu na Nadharia ya Isimu Historia Linganishi, waandishi wanabainisha kuwepo kwa uhusiano wa karibu wa kihistoria baina ya Wapemba na Wamakonde unaotokana na sababu mbalimbali kama vile kuhamahama, kukimbia vita, kuoana na suala la shughuli za uchumi na biashara.

Nao Oliva Mang'ita na Fabiola Hassan wanakuletea makala yanayohusu miundo ya vishiriki vya kitenzi isiyofuata udarajia wa dhima za kisemantiki katika sentensi za Kiswahili. Katika makala hayo, waandishi wanabainisha kuwa, kulingana na udarajia huo, dhima za kisemantiki zinapaswa kupangwa kuanzia nafasi ya juu (kushoto) hadi nafasi ya chini (kulia), ambapo dhima ya juu inapaswa kuwa kiima cha sentensi. Hata hivyo, kuna miundo inayokiuka utaratibu huu, ambapo dhima za chini zinahusishwa na kiima badala ya dhima za juu. Makala haya yanaonesha miundo mbalimbali isiyofuata udarajia, ikiwemo <kimahali, kithimu, (mtenda)>, <kiala, (mtenda)>, <kimahali, kithimu>, <kiathirika, (mtenda)>, <mhis, (mtenda)>, <kiathirika, kiala, (mtenda)>, <kithimu, kimahali, (mtenda)>, <mtenda & kiathirika> na <mtenda & kiathirika/mnufaika>. Aidha, makala yanaonesha kuwa kuna upandishaji hadhi wa dhima zilizopo chini katika udarajia pamoja na Ikupendekeza kufanyika kwa utafiti zaidi ili kubaini sababu za miundo hii kutofuata udarajia wa dhima za kisemantiki.

Kwa upande wa makala za fasihi, watafiti wamejitokeza katika maeneo mbalimbali ya kitaaluma na kushughulikia baadhi ya nyuga. Makala ya Mugwe Mwaniki, Omboga Zaja, na Rayya Timammy yanachunguza uakisikaji wa udongo

kama dhana ya kiikolojia katika ushairi wa Kiswahili, hususan tingo za Mohammed na Mberia. Waandishi hawa wanabainisha kuwa udongo unaakisi masuala ya kitamaduni, kiroho, na thamani za kiikolojia, ukionyesha mahusiano ya kina kati ya binadamu na mazingira asilia. Mashairi yanayohusisha udongo kwa lugha ya kiishara yanauchora kama shahidi wa juhudini na mahangaiko ya binadamu katika kuleta upatanifu na mazingira, huku pia yakionya dhidi ya matumizi hatarishi ya rasilimali za asili na uchafuzi wa mazingira. Mjadala umeegeemezwu katika Nadharia ya Uhakiki wa Kiikolojia ya Glotfelty (1996), inayochambua mwngilio wa binadamu na mazingira katika fasihi. Uchanganuzi unaonyesha athari chanya na hasi za mienendo ya binadamu kwa ikolojia kupitia visa na lugha ya kiishara.

Martina Duwe, kwa upande wake, ameandika makala yanachunguza thamani ya “Mla” katika methali za Kiswahili na jinsi methali hizo zinavyodokeza maarifa ya kimaadili yanayozingatia kaida za jamii ya Waswahili. Uchambuzi umefanywa kwa kutumia Nadharia ya Uhalisia na mbinu ya uchambuzi matini. Katika makala haya imeoneshwa kuwa methali zenye kumrejelea Mla zinasisitiza vipengele vya mbalimbali vya kimaadili. Aidha, imebainishwa kuwa methali zinazomrejelea “Mla” zimeundwa kwa ufundi ili kuhimiza maadili yanayofaa kwa maisha ya jamii ya Waswahili, zikibeba maarifa yenye umuhimu kwa kuhifadhi utamaduni wao.

Nao Winfrid Mligo, Aldin Mutembei, na Ramadhani Thomas Kadallah wamekuletea makala inayochunguza mtagusano baina ya hisia na motifu, wakitoa mifano kutoka tamthilia ya *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe*. Uchunguzi umefanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji matini na kuongozwa na Nadharia ya Rasa. Matokeo yanaonesha kuwa motifu huibuliwa na hali ya kujirudiarudia kwa matendo, ambapo hisia za wahusika zinachochea hali hiyo. Hivyo, kuna uhusiano wa karibu kati ya hisia na motifu, kwani hukamilishana na kujenga maudhui ya matini fasihi.

Naye Waithiru Kago Antony ameandika kuhusu urithi wa vivuli vya utawala wa kikoloni kwa kutumia riwaya *Nguu za Jadi* ya Clara Momanyi. Uchanganuzi umeongozwa na Nadharia ya Baadaukoloni na umebainisha nyuzi mbalimbali zinazoonyesha athari za ukoloni mamboleo kama vile ubaguzi, unyamazishajji, ujisadi, na uongozi mbaya. Makala yanaonesha kuwa madhara ya ukoloni bado yanaathiri jamii za Afrika kupitia udhibiti wa viongozi wa mataifa ya ulimwengu wa tatu na utegemezi wao kwa mataifa ya ulimwengu wa kwanza. Mfumo huu unaendeleza ubawa wa kibeberu licha ya uhuru wa kisiasa wa mataifa hayo.

## **Wahariri**

Disemba 2024

**WAANDISHI WA MAKALA MULIKA NA. 43 (2)**

<b>Na.</b>	<b>Jina</b>	<b>Taasisi</b>
1	Tumaini Mahendeka na Luinasia E. Kombe	Taasisi ya Elimu Tanzania & Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam
2	Mogden Chisia, Iribi Mwangi, Ayubu Mukhwana, na Hezron Mogambi	Chuo Kikuu cha Nairobi
3	Anold Kamugisha	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
4	Pendo Mwashota na Mussa Hans	Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa & Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
5	Oliva Mang'ita na Fabiola Hassan	Chuo Kikuu cha Dodoma
6	Mugwe Mwaniki, Omboga Zaja, na Rayya Timmamy	Chuo Kikuu cha Nairobi
7	Martina Duwe	Chuo Kikuu Mzumbe
8	Winfred Mligo, Aldin Mutembei, na Ramadhani Thomas Kadallah	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
9	Waithiru Kago Antony	Chuo Kikuu cha Laikipia